

Jina: Nambari:

Sahihi ya Mtahiniwa

Tarehe:

102/3

KISWAHILI (FASIHI)

Karatasi ya Tatu

Julai/Agosti 2013

MUDA: SAA 2¹/₂

MTIHANI WA MWIGO WA SHULE ZA WILAYA YA NYANDO

Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)

KISWAHILI

Karatasi ya Tatu

Julai/Agosti 2013

SAA 2¹/₂

MAAGIZO:

1. *Jibu maswali MANNE pekee*
2. *Swali la kwanza ni la LAZIMA*
3. *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Ushairi , Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi na Fasihi simulizi*
4. *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

SEHEMU YA A: USHAIRI

1. soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata

1. Yawile matononofu majani hali yoyote iwavyo

Yefura ukamilifu majani yalikiota vilivyo

Pamoja yalimakifu majani kwa jinsi mambo yendayo

Fahali kayatilifu majani ndivyo igeuke sivyo

Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

2. Ingawa yali dhaifu majani pamoja yalishikana

Ama katika wakifu majani au kwa kusaidiana

Ndugu yali bainifu majani tokea zamani sana

Yakapondwa bila hofu majani fahali walipowana

Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

3. Pondaponda mepondeka majani fahali wakivutana

Tena yakatawanyika majani kwa jambo lisilo kina

Yakabaki kudhiika majani ndugu wanaofanana

Fahali wanayacheka majani wala habri hawana

Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

4. Fahali wanapotaka yakini hata hutembeleana

Na makoo kadhalika yakini wanapotoka kuonana

Ndama pia watavuka yakini ng'ombe ile kulishana

Tena nyasi hazochoka yakini karibu kazikutana

Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

5. Si ndaama si ukoka majani si mbuga si wanda tena

Yamebaki mabaka majani vipande kuoteana

Kwa machaka hazoshika majani hayawezi kupachana

Na fahali watimka majani'ngali wakisuguana

Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

Maswali

- (a) Mwandishi ana ujumbe gani katika shairi hili? (al. 2)
- (b) Eleza muundo wa shairi hili. (al. 4)
- (c) Mwandishi amefauluje katika kutumia uhuru wa kishairi? (al.3)
- (d) Huku ukitoa mifano **miwili** eleza mbinu za uandishi alozotumia mwandishi (al. 2)
- (e) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathari (al. 4)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi (al. 3)
- (i)Matonofu
- (ii)Mabaka
- (iii)Kupachana
- (g) Taja bahari zozote **tatu** za shairi hili (al3)

SEHEMU YA B : RIWAYA

S.A Mohamed : Utengano

Jibu swali la 2 au 3.

2. “ Stahimili bwana , stahimili bwana, utayaharibu mambo.”

- (a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al.4)
- (b) Fafanua kwa ufasaha sifa za mnenaji (al. 4)
- (c) Eleza matukio yaliyotokea baada ya dondoo hili (al.5)
- (d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili (al.1)
- (e) Jadili mabaya yaliyotekelezwa na mrejelewa katika hadithi ya utengano (al.6)

AU

3. Juhudi za wanawake kujikwamua zinasambaratishwa na wanawake wenyewe. Jadili kauli hii ukirejelea riwaya ya utengano (al.20)

SHEMU YA C: TAMTHILIA

Timothy M. Arege; Mstahiki Meya

Jibu swali la 4 au 5

“Sisi wafanyakazi tuna matatizo mengi yaliyotuzonga kwa muda mrefu. Kwanza mishahara yetu midogo”

- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (al. 4)
- b) Kauli hii ilitolewa na nani (al.2)
- c) Taja na ueleze kwa kifupi matatizo mengi yaliyoikabili jamii inayosawiriwa katika tamthilia hii (al.6)
- d) Utatuzi wake ulikuwaje ? (al.8)

AU

- 5. Uozo wa kijamii umetamalaki katika eneo la cheneo. Thibitisha (al.20)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

Ken Walibora na S. Mohamed ; Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine

Jibu swali la 6.

- 6. Ubaguzi umekita mizizi katika Diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine. Huku ukirejelea hadithi zozote tano , jadili ukweli wa kauli hii. (al.20)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 7

- 7. (a)Taja na ueleze sifa zozote tano za ngano (al.5)
- (b) Taja fomula zozote mbili za ufunguzi kisha ueleze umuhimu wake katika utanzu wa hadithi (al.10)
- (c) Miviga ni nini? (al.2)
- (d) Eleza sifa zozote tatu za mivigha (al.3)